

102/3
KISWAHILI
KARATASI YA TATU
(FASIHI)
JULAI/AGOSTI, 2013
MUDA: SAA: 2½

MTIHANI WA MWIGO – WILAYA YA KIHARU/KAHURO
KIDATO CHA NNE - 2013

Hati Ya Kuhitimu Kisomo Cha Sekondari

MAAGIZO:

1. Jibu maswali **manne** pekee.
2. Swali la **kwanza** ni la **lazima**.
3. Maswali hayo mengine **matatu** yachaguliwe kutoka sehemu **nne** zilizobaki.
4. Usijibu maswali **mawili** kutoka sehemu **moja**.
5. Kila swali lina alama **20**.
6. Mtihini huu alama **80**.

SEHEMU A: USHAIRI

SWALI LA LAZIMA:

1. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali:

Ajaye kisimani mbele, hunywa maji maenge,
Asinywe yalo na vunju,
Yakampa kigegezi
Yakamtibua roho akaona na kinyaa,
Awali ndio awali awali mbovu hamna.

Ikiwa utalimatia,
Utayaramba makombo,
Uvidata vitu cheche
Kisoma aali kikupe kisogo,
Inajuzu ujihimu
Mwanafuu darasani
Uraukapo bukrata
Katu hutayaramba makombo
Hutokosa kisebeho.

Dereva nawe utingo,
Natija ni asubuhi,
Wateja utawawahi,
Wasaa kuzingatia,
Uwafikishe kazini,
Kwa wasaa ufaao,
Wasije wakateteshwa na
bosi wao nao wakuapize

Nawe mwanazaraa,
Mpini uukamate kabla,
Jua kutiririsha majasho jasadini,
Ushindwe kung'oa magugu,
Kutoka kwa lako konde.

Mhadimu mwenye zohali,
Yajuzu ujihimu
Maziwa ununue majogoo
Usije ukayadata na hivyo

Ukaandaa chai mkandaa
Wateja wakuambae mithili ya ibilisi.

Kiswahili Karatasi ya Tatu

2

MASWALI

- (a) Shairi hili ni la aina gani? Elezo. (alama 2)
- (b) Eleza nasaha yoyote inayotolewa kwa wafanyakazi wowote watatu. (alama 3)
- (c) Je, wafanyakazi waliolengwa na mshairi wataathirika vipi endapo hawatafuata ushauri wanaopewa kwenye shairi? (alama 3)
- (d) Kwa mujibu wa mshairi, mwanafunzi anahimizwa kurauka mapema kwa nini? (alama 2)
- (e) Tambua tamathali zozote **mbili** za semi zilizotumiwa na mtunzi. (alama 2)
- (f) Taja sifa zozote **mbili** za kimuundo zilizotumiwa na msanii. (alama 2)
- (g) Andika ubeti wa kwanza kwa lugha nathari. (alama 3)
- (h) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika kwenye shairi. (alama 2)
- (i) Wakuapize
- (ii) Jasadini
- (i) Onyesha matumizi yoyote ya mstari mshata. (alama 1)

SEHEMU B: TAMTHILIA: MSTAHIKI MEYA (T. Arege)

2. Eleza ufaafu wa anwani ‘Mstahiki Meya’. (alama 20)
3. Tamthilia ya Mstahiki Meya ni taswira kamili ya matatizo yanayokumba mataifa mengi barani. Afrika. Fafanua ukirejelea hadithi hii. (alama 20)

SEHEMU C: RIWAYA: UTENGANO (S.A. Mohamed)

4. “Nataka nikueleze hivi darlin--- aliinua uso, akamtazama mwenzake. ‘Unajua watu wakikaa pamoja kama vilivyo visahani, hugongana ...’”
- (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

- (b) Taja mambo yoyote mzungumziwa aliambiwa kabla na baada ya kusemwa kwa maneno haya. (alama 11)
- (c) Msemaji wa maneno haya alikuwa ni katili asiye na maadili. Taja ukatili huo. (alama 3)
- (d) Onyesha mbinu yoyote moja inayojitokeza kwenye dondoo. (alama 2)

AU

5. Kwa kurejelea ndoto zilizotumika kwenye riwaya hii fafanua yaliyomo kisha uelezee tafsiri yake. (alama 20)

Kiswahili Karatasi ya Tatu

3

SEHEMU D: HADITHI FUPI (Damu Nyeusi Na Hadithi Nyingine)

6. Glasi ya Mwisho Makaburini – S. A. Mohamed
“Umebaki kulala kochini kama mgonjwa wa malaria. Au ndiyo huendi: Yaani umegoma?... imani yako imekutawala vilevile au siyo?
- (a) Eleza muktadha wa dondoo hii. (alama 4)
- (b) Ni imani ipi inayorejelewa? (alama 3)
- (c) Eleza msimamo wa mnenaji kuhusu imani hii. (alama 3)
- (d) Taja mbinu zozote **nne** za lugha zinazotumika katika dondoo hili. (alama 4)
- (e) Fafanua sifa zozote **tatu** za msemewa wa dondoo hili ukirejelea hadithi nzima. (alama 6)

AU

7. **Maeko – M.K. Ghassany**

- (a) Taja na ufafanue madhara yoyote **matano** ya ulevi katika hadithi ya ‘Maeko’. (alama 10)
- (b) Eleza sifa na umuhimu wa Jamila katika hadithi ya ‘Maeko’. (alama 10)

SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI

8. (a) Ni nini maana ya miviga. (alama 2)

- (b) Eleza sifa zozote **sita** za miviga. (alama 12)
- (c) Taja njia zozote **sita** zinazotumiwa na jamii ya kisasa ili kuendeleza Fasihi Simulizi. (alama 6)

ANSWERS:

Order a copy of answers from www.schoolsnetkenya.com/order-e-copy

NB> We charge Kshs. 100 ONLY to meet website, e-resource compilation and provision costs